

## **Je, mimi ni msichana Albino ninaweza kupata mimba kama nikijamiiana mara moja tu?**

By SW - Melkisedeck Shine · April 15, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Ndiyo msichana anaweza kupata mimba kwa kujamiiana mara moja tu bila kujali ana rangi gani ya ngozi. Wasichana weupe, weusi na wanaoishi na ualbino au wasio na ulemavu wa ngozi wanafanana wote inapokuja kwenye suala la uwezekano wa kupata mimba. Kinachobainisha/ kinachosababisha upatikanaji wa mimba ni wakati tendo la kujamiiana linapofanywa na hatua ya mzunguko wa hedhi. Kama yai lililopevuka kwa ajili ya kurutubishwa litakuwa tayari basi ujauzito utatokea mara tu baada ya mbegu ya mwanaume kuingia, (wakati wa kujamiiana). Ujauzito unaweza kutokea hata kama msichana alikuwa bado bikira na ni mara yake ya kwanza kujamiiana.

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=25557>